TANGAZO LA SERIKALI NA. 593 la tarehe 30/9/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) (g) na16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA NSIMBO ZA MWAKA 2022.

Jina la Sheria Ndogo Tangazola Serikali Na. 102 ya 2017

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria ndogo za (Ada na Ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya Nsimbo 2022 na zitasomwa pamoja na Sheria ndogo (ad na ushuru) za

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za mwaka 2017 ambazo zitajulikana kama sheria Ndogo kuu.

Marekebisho ya kifungu cha 8

2. Marekebisho yanafanyika katika Kifungu cha 8cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza aya ya (g) na (h) ambazo zitasomeka kama ifuatavyo:-

(g) atakayeuza bidhaa ya aina yoyote nje ya masoko au maeneo yaliyoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya biashara; au

(h) atakaidi kuingiza gari la biashara eneo la stendi au maegesho.

Tangazo la Serikali Na.



3. Marekebisho yanafanyika katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo kuu kwa:-

i) Kufuta aya ya kumi kuhusiana na ada ya

kuchangia uzoaji taka mijini (emerging towns) inafutwa.

ii) Kufuta aya ya kumi na moja kuhusiana na ushuru wa mazao inafutwa.

iii) Kuongeza ki en ele cha 4 hadi cha 11 kama ifuatav o:-

4. ushuru wa TZS 20,000 kwa mwezi kwa wamiliki wa mashine za kusa a mawe a madini crusher .

5. ushuru wa TZS 10,000 kwa gari moja kwa mfan abiashara wa chuma chakavu.

6. ada ya TZS 20,000 ya usajili wa kikundi na ada ya TZS 10 000/- a kuhuisha usaiili kwa kila mwaka kikundi kinapotaka kuhuisha usaiili.

7. ada ya TZS 20,000 kwa ajili ya kibali cha kuingia oorini kufanva shuohuli za ufiigaji nyuki.

8. ada ya TZS 500 kwa kila mzinga wa kisasa kwa anavesafirisha kwenda nie na ndani ya Halmashauri.

9. Ushuru wa nyumba za kulala wageni utakaotozwa kwa 10% ya bei ya kila chumba kitakacholipiwa na mteia.

10. Ada ya leseni za biashara itakayotozwa kwa kuzingatia viwango vilivyopo kwenye Sheria ya Leseni za biashara.

11. Ushuru wa mazo ya misitu utatozwa kwa mnunuzi kwa kiwanqo cha 5% va bei va kununulia.

iv) Na kurekebisha Aya ya kumi na mbili iii kusomeka aya ya kumi baada ya aya ya kumi na kumi na moja kufutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 9

4. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo kuu kwa kukifuta na kukiandika upya kama ifuatavyo:-

(9) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) na isiyozidi shilingi milioni moja (1000,0000) au kutumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au kutumikia adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Marekebisho ya kifungu cha 10

5. Marekebisho yanafanyika katika Kifungu cha 10 cha sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya kama ifiatavyo:-

(10) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya kiasi cha shilingi laki mbili (200,0001=) Mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatishwa katika Sheria Ndogo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo iliwekwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 27-28 Aprili, 2021 na kubandikwa mbele ya:-

MOHAMED RAMADHANI
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya Nsimbo*

HALAWA MALENDEJA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Nsimbo*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
19 Septemba, 2022

INNOCENT L. BASHWANGWA (MB),
*Waziri wa Nchi -OR-TAMISEMI.*